
# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 18 | Januari 1, 2023 NAKALA BILA MALIPO


# USHURU WAGONGA MAHASLA

**Mzigo mkubwa wa deni la Kenya umesukuma serikali kung'ang'ana kuongeza mapato ya ushuru, huku kiwango cha ushuru wa faida ya mapato kikipanda na kufikia asilimia 15 kuanzia leo. Hata hivyo, wataalamu wanaonya kuwa huenda mpango wa kupanua mawambo ya ushuru hautafaulu bila ongezeko la ajira, uzalishaji na uwekezaji.**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe

> ***epaper.nation.africa.***




Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyo-

**6 KENYA HATARINI YA KUSHINDWA KULIPA MADENI:** Mnamo Februari Standard Bank Group, benki kubwa zaidi Afrika, iliorodhesha Kenya miongoni mwa nchi tano barani zilizo hatarini kubwa ya madeni. Je, Kenya itafuata mwelekeo wa Ghana?

**8 KUZIMA WANASIASA WABINAFSI:** Baada ya Raila kurudi upande anaofahamu vyema na kuapa kuongoza mageuzi ya kikatiba kupitia baraza la kikatiba, naye Rais Ruto akitaka bunge lishughulikie jambo la hilo, ni lazima juhudi za ubinafsi zipingwe.

**11 JINSI WENYE NGUVU HUPOROMOKA:** AMahakama ya Angola yaamuru kutwaliwa kwa mali ya dola 1 bilioni ya Isabel dos Santos, aliyekuwa mwanamke tajiri zaidi Afrika.



**13 CHINA YAZUA HOFU DUNIANI:** Uamuzi wa Beijing wa kulegeza masharti wakati wa maambukizi makubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa yatia ulimwengu tumbojoto.

# Tuongeze uzalishaji na mapato kwanza ili ushuru zaidi upatikane

Mojawapo ya sifa za utawala wa Kibaki ni kwamba serikali ilikuwa imedhibiti mapato na matumizi ya pesa. Wizara ya fedha haikutegemea sana madeni ya ndani ya nchi kuepuka kuzuia biashara kupata mikopo huku Benki Kuu ya Kenya (CBK) ikihakikisha benki, ambazo zililazimika kukopesha watu na biashara zilinawiri, na haikusababisha shinikizo zinazoweza kuleta mfumko wa bei za bidhaa.

Hatua hii ilisababisha hali ambapo taasisi za kifedha ambazo awali zilijivuta kuruhusu watu wa mapato ya chini kufungua akaunti kuanza "kuchuuza" mikopo isiyo na dhamana kwa wafanyakazi waliokuwa na mishahara, biashara ndogo na makampuni. Hii, pamoja na udhibiti mkali wa CBK, zilichochea ukuaji, kubuni nafasi za ajira kwa kuwa kampuni zilipanuka na mapato kuongezeka.

Ni mseto huu wa uchumi, wataalamu wanasema, ambao uliweka msingi wa ukuaji mkubwa ambao kufikia leo unasifiwa kama kumbukumbu isiyoweza kufutika ya utawala wa Kibaki.

Kukiwa na rasilimali za upanuzi na mazingira yanayofaa ya uchumi mkubwa, wataalamu hao wanatufahamisha kuwa, kampuni mpya zilichipuka huku zilizokuwepo zikipanuka, na kuinua uzalishaji na kuunda nafasi zaidi za ajira. Hii, bila shaka, ilifanya mapato kuwa zaidi kwa mkusanyaji ushuru.

Tuangalie hali mwanzo wa mwaka wa 2023. Kwanza, hali ya uchumi ni tofauti kabisa, kumaanisha kuwa hata kuiga uchumi wa Kibaki hakuwezi kuibadilisha. Wataalamu



Henry Munene

Ingawa kubadilisha madeni na kuimarisha ukusanyaji ushuru ni hatua muhimu za muda mfupi, aina ya ukuaji unaonuiwa kubadilisha Kenya kuwa nchi ya mapato ya juu - inavyoeleza Ruwaza ya 2030 na miongozo mingine ya kitaifa - kutahitaji viwango vya juu vya uzalishaji ili kuongeza mapato, kubuni nafasi mpya za ajira, kuinua sekta muhimu kama vile utengenezaji wa bidhaa na kilimo na hatimaye kuwa na akiba ya kuwekeza.

sasa wanaonya kuwa huku mfumko ukiendelea kuongezeka kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu, na kupungua kwa thamani ya shilingi kukiongeza presha kwa ulipaji wa madeni, kuna haja ya waundaji wa sera katika serikali ya Ruto kupanua mawazo yao.

Kukumbatia mabadiliko ya kuacha mikopo ya muda mfupi ambayo ni ghali hadi ya muda mrefu ambayo ni nafuu ni sawa, lakini je, kuna nafasi ya hiyo nafuu kweli? Pili, pupa ya kupanua mawambo ya ushuru na kuleta walipa ushuru wengi inaonekana kuwa nzuri. Hata hivyo, kama wataalamu hata katika toleo hili wanavyosema, kupanua mawambo ya ulipaji ushuru kutaleta manufaa tu iwapo nafasi za ajira zitaundwa, uzalishaji kuongezeka na uwekezaji zaidi kuelekezwa kwa uchumi.

Hali mbaya ya kiuchumi imezidishwa na uvamizi wa Urusi nchini Ukraine amabo ulileta shida ya kuagiza chakula kutoka nje kufuatia ukame wa muda mrefu ambao uliacha Wakenya wapatao milioni nne wakikumbwa na njaa.

Licha ya hayo, hakuna njia ya mkato ya kufufua uchumi kwa Kenya. Ingawa kubadilisha madeni na kuimarisha ukusanyaji ushuru ni hatua muhimu za muda mfupi, aina ya ukuaji unaonuiwa kubadilisha Kenya kuwa nchi ya mapato ya juu - inavyoeleza Ruwaza ya 2030 na miongozo mingine ya kitaifa - kutahitaji viwango vya juu vya uzalishaji ili kuongeza mapato ya nchi, kubuni nafasi mpya za ajira, kuinua sekta muhimu kama vile utengenezaji wa bidhaa na kilimo na hatimaye kuwa na akiba ya kuwekeza.

Hilo likifanyika, kupanua mawambo ya ukusanyaji ushuru na hata kuongeza mara nne mapato ya ushuru kutakuwa rahisi kutekekeza.

*hmunene@ ke.nationmedia.com*

***- Imetafsiriwa na Benson Matheka***

Darubini ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Wafurahia kandanda kwa michoro mwilini



Mshambuliaji wa Argentina Lionel Messi abusu tuzo ya Kombe la Dunia wakati wa sherehe ya kutoa tuzo za Kombe la Dunia Qatar 2022 baada ya mechi ya fainali kati ya Argentina na Ufaransa katika Uwanja wa Michezo wa Lusail, mnamo Desemba 18, 2022. PICHA | AFP

# Tattoo tele Messi akitarajiwa kustaafu

Mashabiki wa timu ya Argentina iliyonyakua kombe la kandanda nchini Qatar mwezi huu wamepiga foleni jijini Buenos Aires kwa michoro ya mwilini (tattoo) ya nahodha wa timu hiyo Lionel Messi na Kombe la Dunia."Katika wiki mbili zijazo,nina (shughuli) kuhusu Kombe la Dunia,"mchoraji wa tattoo Esteban Vucinovich akaambia AFP katika mji huo kuu.

"Baadhi ya watu walikuwa wamepanga kuchorwa nyoka ama mafuvu ya kichwa lakini sasa wanabadilisha kuchorwa Messi au Kombe. Ninahudumia watu wawili au watatu kwa siku," akasema.

Mchoro unaotakiwa na wengi ni wa Kombe, akasema Vucinovich, ukifuatiwa na wa Messi kisha golikipa Emiliano Martinez, aliyechangia sana ushindi wa timu hiyo katika mechi ya fainali dhidi ya Ufaransa.

Mashabiki wengi wanavutiwa na michoro waliochorwa baadhi ya wachezaji wa Argentina kama vile Angel Di Maria, ambaye hivi majuzi alichorwa tattoo mguu wa kulia. "Nilichorwa tattoo ya Messi kama ishara ya shukrani,"mtumishi wa umma Nicolas Rechanik akaambia AFP."Mchoro huo unawakilisha Hii sio tu nafsi ya Messi lakini pia timu iliyotuletea Kombe la Dunia la tatu na miaka yote waliyojitahidi kufikia lengo hilo."


Kabla ya kuchorwa picha ya Messi akiwa na jezi ya mistari ya samawati na myeupe akibusu kombe kwenye mguu wake wa kushoto, Rechanik alikuwa tayari amechorwa mchoro mwingine wa nyota wa kandanda wa Argentina - Diego Maradona."Ni picha halisi ya hali ya kandanda ya Argentina na maana ya kuwa raia wa Argentinea," akasema.

■ Ni msanii aliyefanikiwa kwa bidii yake

# Mjukuu wa Bob Marley aaga dunia

Mwanamziki Joseph "Jo Mersa" Marley, mjukuu wa Bob Marley na msanii maarufu kutokana na juhudi za kibinafsi, ameaga dunia akiwa na umri wa miaka 31, ripoti kutoka Amerika zimesema.

Mwakilishi wa Marley, mzaliwa wa Jamaica, alithibitisha kifo chake kwa Rolling Stone, lakini hakusema kilichokisababisha. Radio ya WZPP jijini Miami, ambako msanii huyo alitumia muda mwingi wa maisha yake, iliripoti kuwa alipatikana ndani ya gari baada ya kuugua maradhi ya pumu Jumanne.



Bob Marley PICHA | MAKTABA

Waziri Mkuu wa Jamaica Andrew Holness alisema kupitia Twitter kuwa "alihuzunishwa sana" na habari za kifo chake, na akatuma risala za rambirambi kwa wazazi wa Marley, Stephen na Kerry. "Rambirambi zangu za dhati ziwaendee marafiki na washirika wa Joseph ikiwemo jamii na mashabiki wa muziki wa Reggae kila mahali," akasema.

Marley alizindua albamu yake ya kwanza, Comfortable, mnamo 2016 kisha Eternal mnamo 2021. Akihojiwa na Rolling Stone mnamo 2014 Marley alizungumza kuhusu malezi yake miongoni mwa wanamziki, akiwemo baba yake na mjomba wake Ziggy. "Ilikuwa furaha kubwa kwangu kuona watu hao wakija nyumbani na jinsi walivyofanya kazi yao," akasema wakati huo.

"Nilikuwa nikijaribu kufanya kazi ya ziada nyumbani baada ya kutoka shule lakini nilitekwa na waliyokuwa wakifanya ndani ya studio na kwenda kuchungulia."

Alisema licha ya asili yake ya muziki, daima alitaka kuchukua mkondo wake mwenyewe. "Mpango wangu ni kufanya jambo jipya nikitumia asili yangu." akaambia Rolling Stone. Radio ya WZPP iliripoti kuwa Marley amemacha mke na binti.

■ Chaguzi za seneti, bunge na wadi

# Wapiga kura kurudi katika debe



Wapiga kura wa maeneo manne ya uchaguzi Alhamisi, Januari, 5, 2023 watarudi debeni kwa uchaguzi mdogo wa wawakilishi wao.

Kiti cha seneta wa Elgeyo Marakwet kilibaki wazi baada ya Seneta Kipchumba Murkomen kuteuliwa Waziri wa Barabara, Uchukuzi na Utumishi wa Umma katika baraza la mawaziri la Rais William Ruto. Viti viwili vya ubunge pia vilibaki wazi baada ya Alice Wahome (Kandara) na Aden Duale (Garissa Township) kuteuliwa Mawaziri wa Maji, Usafi na Unyunyiziaji na Ulinzi mtawalia. Uchaguzi mdogo wa nne ni katika Wadi ya Shella Kaunti ya Lamu.

■ Madai yanajumuisha kukosa vifaa vya kazi

# Madaktari kugoma kutetea maslahi



Madaktari wanatazamiwa kusitisha huduma zao katika hospitali zote wiki hii wakilalamikia hatua ya Wizara ya Afya ya kutotimiza mkataba wa 2017-2021 kuhusu mishahara.

Hatua hiyo huenda ikavuruga huduma za afya kote nchini.

Walikuwa wametoa notisi ya siku 30 Novemba 28, 2022 kuhusu nia ya kugoma huo kama serikali ingekataa kusikiliza tetesi zao.

Wanasema vyumba maalumu, wakufunzi wa utabibu, kuajiriwa kwa madaktari zaidi, vifaa vya kazi na nyongeza ya mishahara ni miongoni mwa mahitaji ambayo hayajatimizwa.

***- Zimetafsiriwa na Mary Wangari***

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ UKUSANYAJI USHURU

# MZIGO MZITO WA USHURU




**Jumba la Times Tower jijini Nairobi, makao makuu ya Mamlaka ya Ushuru Kenya.** PICHA I MAKTABA

## Serikali bado haijawezesha Wakenya kuwa na mapato mazuri yanayofaa kuongeza ushuru

● Na Dkt Mbui Wagacha

Makala haya yanaangazia ongezeko la viwango vya ushuru wa rasilimali na uuzaji wa hisa, kutoka asilimia tano mwaka wa 2022, hadi asilimia 15 kuanzia Januari 1, 2023. Ushuru wa rasilimali ulirudishwa mnamo 2015 baada ya kusimamishwa 1985. Ongezeko hili jipya linajadiliwa dhidi ya maelezo kuhusu ushuru wote na uwezo wa mlipa ushuru na mfumo wa ushuru nchini Kenya.

Utozaji wa ushuru unakaidi usahihi licha ya tafiti nyingi na ufahamu. Ushuru wa ongezeko la rasilimali, hasa, ni mageuzi ya kunyonya tabaka la wawekezaji. Mkosaji mkuu hapa ni hali yetu ya mfumko. Mfano rahisi wa familia mbili unaonyesha kuwa familia changa inayonunua nyumba Januari 1, 2022 kwa Kh50 milioni, ikitarajia kuingia nyumba hiyo miaka kumi ijayo, na familia inayokaribia kustaafu inayotaka kuuzia nyumba katika miaka kumi kuwa na mapato baada ya kustaafu, familia zote mbili zinapoteza mapato.

Huku hali ya mfumko Kenya ikiendelea kuongezeka kwa asilimia 4 na kupungua kwa thamani ya shilingi kwa wakati huo, na thamani halisi ya nyumba hiyo ikikosa kubadilika, familia hiyo inalipa ushuru wa asilimia 9.7 kwa mali ambayo faida yake ni sufuri. Mstaafu anayeiuza anaingia maisha ya uzeeni akiwa maskini zaidi baada ya kulipa ushuru kama huo kwa faida ya mali ambayo kwa kweli haipo. Sera ya kutafuta mapato Kenya na katika nchi zingine kila wakati huwa ngumu.

Ni nchi chache zinazoweza kujivunia kazi yake na kuafikia kikamilifu mapato zinayolenga. Wakati huo huo mazingira yasiyofaa ya kutumiwa kwa mazingira ya kutoza ushuru hayafanani yakilinganishwa na makosa ya mbinu za mkusanyaji ushuru.

Sera pevu zinahitaji kuhesabu gharama ya jamii na manufaa, na pia yaliyofichwa kwa kila tukio (ni nani anayelipa ushuru kati ya mtumiaji na mzalishaji?). Baadhi ya dhana zinakaidi hesabu ya haraka kwa kulazimisha au kubadilisha viwango.

Fikiria kuhusu mzigo wa ziada wa ruzuku ambapo changanuzi zinathibitisha kuwa gharama inazidi manufaa kwa jamii. Au ushuru wa mapato, ushuru wa leba ambao unasababisha mzigo wa ziada pia. Hali nyingi zinaweza kutolewa kama mfano.

Katika hali ya sasa Kenya, baadhi ya watungaji wa sera wanatazama shimo la miradi lililochimbwa miaka ya majuzi, huku baadhi ya pesa zikifujwa na kuporwa kwa siri, kisha wanatazama kuongezeka kwa madeni ambayo walipa ushuru wanapaswa kulipa bila kuwa na pesa.

Kisha wanaona watu wengi maskini au wasio na kazi nzuri walio na mapato ya chini na wanaamua 'kupanua mawambo ya ushuru', tamko la kupunguza gharama ya ukusanyaji ushuru, kuwa na watu wengi wanaolipa ushuru na kusaidia kupunguza viwango vya ushuru kwa jumla.

Ni mtego rahisi unaoweza kunasa, kama watawala wa kikoloni wa zamani nchini Kenya, ambao waliweka ushuru wa nyumba kwa walipa ushuru bila juhudi zozote za kuwapa shughuli za kiuchumi, uzalishaji au ajira.

Hivyo basi, mababu wetu walilipa ushuru kupitia kazi ya lazima kwa kuacha kazi walizotegemea kujikimu au kupitia mifugo wao. Kisha wakoloni walifadhili miradi yao kwa kufungua nchi yetu (ilikuwa makao yao wakati huo) na kufanya kazi kwa walowezi wa kikoloni katika ardhi walioyopokonywa.

Heri njema kwa watungaji hao. Shida ni kuwa, kama wakoloni waliowatangulia, serikali bado haijafanya kazi kubwa inayohitajika kuwezesha raia wake kuwa na mapato mazuri, mapato ya kibiashara, na pesa za matumizi zinazofaa kuongeza kwa kiwango kikubwa mapato ya ushuru kwa serikali ya kitaifa au serikali za kaunti.

Mzigo wa ziada unaweza hata kuashiria kuwa bidii kazini inaweza kupungua kutokana na kuongezeka kwa ushuru.

Hivyo basi, kwa kuwezesha uchumi wetu kufufuka baada ya 2022 majibu hayamo katika utashi wa kukopa na kubadilisha madeni ya humu nchini na ya nje, lakini yamo katika kujenga upya uchumi wa kweli. Kwa kufanya hivyo, hakuna kuepuka utekelezaji wa mseto wa sera kuu inayoongeza uwekezaji, uzalishaji, ajira na mapato, kisha kufanya mabadiliko kuelekea kuongeza mapato ya ushuru.

Mfumokazi wa ushuru unafaa kulenga utendaji na kuwa endelevu (ulinganishwe na mapato ya chini na ya juu). Data za Shirika la Taifa la Takwimu Kenya zinaeleza sehemu za mfumo wetu ambazo zinafaa kubadilishwa. Mapato yanaendelea kukosa usawa, ingawa si Kenya pekee.

Watu wapatao 8,300 wanamiliki utajiri unaokaribia wa watu wengine 45 milioni. Asilimia 10 ya matajiri wanapata mara ishirini na tatu zaidi ya asilimia 10 mas-

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Ushuru wa nyumba?

Kutoka Uk 5

kini. Ni asilimia 15 ya watu 2.5 milioni walioajiriwa katika sekta rasmi wanapata mshahara wa Sh100,000. Kwa kuwa mapato katika sekta ya kibinafsi hayarekodiwi, ni vigumu kupata viwango vya chini vya matumizi.

Tuna uchumi ambao data zinaonyesha kuna mabilionea 3,362 ambao wataongezeka hadi 4,274 kufikia 2026, huku tatizo la mapato ya chini likipenya katika sekta rasmi. Ni watu 358,833 (asilimia 15) katika sekta hiyo wanaopata zaidi ya Sh100,000 kwa mwezi, huku 1.18 milioni (asilimia 40) wakipata chini ya Sh50,000, na 57,770 wakipata chini ya kiwango cha kitaifa cha Sh20,123.

Masoko na vituo vyetu vya afya, majumba ya biashara na elimu zimejaa mashine za kutoza ada mapato haya ya chini kwa matumizi ya maegesho mtu akiingia kupata huduma, na hivyo basi kuzidisha umaskini kwa kufyoza mapato haya duni.

Siku hizi, watungaji wa sera wakati mwingine huziba pengo la uzalishaji na ukuaji kwa kutoa onyo kuhusu uhaba wa bidhaa muhimu kama mahindi au mchele, na kuhimiza uagizaji kutoka nje bila kutozwa ushuru kwa kampuni za kusaga, kutengeneza na kuuza sokoni. Kwa sababu ya njaa, baadhi ya raia wanaweza kuchukulia hii kuwa hatua ya kuwasaidia, lakini ni hatari kwao, kama tu ilivyokuwa enzi za wakoloni.

Hii ni kwa sababu onyo hilo huwa la kuunda uporaji kunufaisha maslahi ya biashara za watu binafsi. Matokeo katika hali ya kifedha kisha yanaongeza umaskini na kuumiza uchumi wa Kenya.

Suluhu za sera za uchumi zinazojali raia ni wataalamu wa nchini kutoa ushauri huku wakibadilishana mawazo na wataalamu wa kutoka nje ya nchi. Ufahamu sahihi wa dhana ya kimsingi kuhusu uchumi wa ushuru na katika muktadha wa uchumi, ni muhimu kwa kila swali.

Kwa nini ushuru utozwe na wa aina gani? Kwa sababu utozaji ushuru ndiyo njia ya pekee ya kukusanya mapato, kuendesha serikali na kuwezesha uchumi wa Kenya kuungana na uchumi wa ulimwengu.

Ni vigezo vipi? Utendaji bora, haki (uendelevu|) usawa (watu walio katika nyadhifa sawa wanapaswa kutozwa ushuru kiasi sawa) na gharama ya kuendesha mfumo wa ushuru, unaoitwa gharama ya kusimamia ushuru.

Kwa mfano, Kenya imefanyaje katika utendaji bora? Kiashiria hapa ni ukwepaji wa ushuru ambao watafiti wameripoti. KRA inaweza kuwa na habari za ndani, lakini wakati mwingi inatumia ubaguzi kuhusu ushuru usiokusanywa humu nchini - kama ushuru wa vileo vya humu nchini, hata vyenye ubora wa hali ya juu, huku ikihurumia wawekezaji wa kigeni wanaotengeneza vileo.

Mnamo 2018, shirika la Global Financial Integrityl iliripoti kuwa Kenya inapoteza pesa nyingi za ushuru wa biashara usiokunywa, na likakadiria hasara kutokana na ushuru unaolipwa bila kufikia serikali kuwa dola za Amerika 907, sawa na asilimia 8 ya mapato ya serikali. Mianya hii inageuza mzigo wa ushuru kwa mlipa ushuru wa humu nchini zikiwemo biashara zinazolipa.

Ni kitu gani cha kutoza ushuru mbali na vibanda? Utozaji ushuru unapaswa kuongeza uwekezaji, ajira na uzalishaji, na kusaidia kuongeza ulinganishi wa ushuru na maeneo mengine duniani.

Je, mabadiliko haya mapya yatafufua uchumi? Hesabu iko wazi. Kwanza, hali ya kutegemewa kwa mabadiliko hayo kuleta mapato. Ushuru wa mapato (unaopatikana katika uuzaji) unategemea uamuzi wa anayeuza.

*Dkt Mbui Wagacha ni mwenyekiti wa zamani wa Benki Kuu ya Kenya na mshauri wa rais.*

***-Imetafsiriwa na Benson Matheka***



Mashine ya kielektroniki ya kutoza uhuru (ETR).

■ 'TANO TETE' ZA AFRIKA

## Kenya, Ghana, Ethiopia, Zambia na Angola zamulikwa kuhusu madeni

# KENYA HATARINI YA KUSHINDWA KULIPA MADENI



**Mfanyabiashara katika soko la Muthurwa jijini Nairobi akihesabu pesa baada ya mauzo ya siku mnamo Aprili 19, 2021.**
PICHA I DENNIS ONSONGO.

● CONSTANT MUNDA

Mnamo Februari 2022, Standard Bank Group, benki kubwa zaidi kwa mali Afrika, iliorodhesha Kenya miongoni mwa nchi tano barani zinazokabiliwa na hatari kubwa ya kushindwa kulipa madeni kufuatia mwisho wa ruzuku zilizopewa na nchi tajiri kutokana na janga la corona.

Nchi zingine katika ripoti hiyo, iliyohusu nchi 18 za Afrika, ni Ghana, Angola, Ethiopia na Zambia. Nchi hizi zinajulikana kama "Tano Tete za Afrika" kutokana na mzigo wa madeni.

Neno "tano tete" lilibuniwa kwa mara ya kwanza na mchanganuzi wa masuala ya kifedha katika kampuni ya usimamizi wa uwekezaji Morgan Stanley, mnamo Agosti 2013 kumaanisha uchumi wa Brazil, India, Indonesia, Afrika Kusini na Uturuki. Wakati huo, uchumi wa nchi hizo ulikuwa unaendelea kufufuka kutoka kwa mzozo wa kifedha wa 2008/9 duniani na zilikuwa zikitegemea uwekezaji wa kigeni kufufuka.

Dhana ya "tano tete" imekuwa ikitumiwa katika masoko ya ulimwengu na wachanganuzi tofauti wa kifedha kumaanisha nchi zinazopambana na kuongezeka kwa upungufu wa pesa, kudorora kwa akiba za pesa za kigeni kwa ulipaji wa madeni ya nje na kiwango cha juu cha mfumko, miongoni mwa hatari zingine.

Kwa mfano, mnamo 2017, shirika la kukadiria viwango vya madeni la S & P Global lilichagua

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Argentina, Uturuki, Qatar, Pakistan na Misri kuwa "tano tete" duniani baada ya uchumi wa nchi hizo kuathiriwa vibaya na kuongezeka kwa viwango vya riba duniani wakati huo.

Kwa "tano tete za Afrika", kigezo sawa kimekuwa ni hali mbaya ya mapato kwa uchumi wa nchi hizo huku kukiwa na presha kutoka kwa madeni ya kigeni yanayotimia wakati wa kulipa.

Jibran Qureishi, mkuu wa utafiti wa Afrika katika Standard Bank Group, wakati huo alipendekeza kurekebishwa kwa dharura kwa hali ya kifedha ili kuepuka kupoteza imani ya wakopeshaji wa kimataifa na wawekezaji.

Mzozo wa madeni Ghana ulijitokeza mapema Desemba baada ya uchumi wa nchi hiyo ya Afrika Magharibi kusimamisha ulipaji wa madeni ya kigeni, benki za biashara na mengi ya madeni iliyokopeshwa na nchi zingine.

Hatua ya Ghana, iliyo na utajiri wa dhahabu ya kusimamisha ulipaji wa mingi ya mikopo yake ya kigeni – ya pili Afrika tangu janga lilipotokea baada ya Zambia mnamo Novemba 2020 – imezua mjadala miongoni mwa wanauchumi kuhusu iwapo Kenya inafuatia au la.

Wanaofananisha shida za madeni za Ghana na Kenya wanataja ukosefu wa nidhamu ya kifedha katika nchi hizo mbili katika miaka ya hivi majuzi.

Hii inatokana na upungufu mkubwa wa kifedha ambao umebaki kuwa zaidi ya asilimia tano ya pato la taifa (GDP) – kipimo cha ukuaji wa uchumi- na kusababisha haja ya mikopo kujaza pengo katika bajeti.

Wanauchumi wengi, hata hivyo, wanakumbaliana kuwa Kenya haielekei njia ya Ghana, lakini kuongezeka kwa deni lake kunabaki katika hatari kubwa.

Ghana imetumbukia katika hali hiyo hasa kwa kutoweza kulipa madeni yake ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa miaka mingi kutokana na kuongezeka kwa uhaba wa pesa kulikofikia asilimia 15.29 ya GDP wakati wa janga, kutoka asilimia 3.9 mnamo 2017.

Ili kujaza pengo katika bajeti, nchi hiyo imekuwa ikikopa kwa wingi, na kuongeza mzigo wa madeni kuwa asilimia 76.7 ya GDP mwaka jana na kuzua wasiwasi zaidi kuhusu uwezo wa kuyalipa.

Janga lilisababisha mzozo wa kifedha, ambao mwaka huu ulizidishwa na vita katili vya Urusi nchini Ukraine, kupungua kwa dola katika nchi hiyo ya Afrika Magharibi, ambayo hadi juzi ilikuwa kipenzi cha wawekezaji wa kimataifa. Viwango vya juu vya riba kutokana na mfumko mkubwa 2022, kwa upande mwingine pia vilifungia Ghana – jinsi vilivyofanya kwa chumi zingine zinazoibuka- kutoka masoko ya mtaji ambako ilikuwa ikipata fedha.


Kutokana na hayo, sarafu ya Ghana, cedi, ilishuka dhidi ya dola ya Amerika mwaka huu, na kupoteza asilimia 50 ya thamani yake na kuongeza gharama ya madeni ya kigeni huku gharama ya maisha ikifikia kiwango cha juu zaidi katika miaka 21 cha asilimia 40 mwezi Oktoba.

Hii ilifanya wawekezaji Ghana kudai riba ya zaidi ya asilimia 36.4 kwa mikopo ya miezi mitatu mapema Desemba 2022, mara nne zaidi ya riba ya asilimia 9.37 ambayo Kenya ililipa kwa mikopo sawa.

Wanauchumi wanasema Kenya ilichukua, tofauti na Ghana, Sh297.38 bilioni (dola 2.416 bilioni) kufadhili bajeti kutoka Shirika la Fedha Ulimwenguni zilizotolewa kwa awamu kwa miezi 38 kutoka Aprili 2021, hatua inayopatia wawekezaji imani.

Hadi mwishoni mwa 2022, Rais wa Ghana Nana Akufo-Addo alikuwa akikataa msaada wa IMF, ambao kwa kawaida huwa na masharti makali ya mageuzi ya uchumi ikiwemo kupunguza matumizi. "Tatizo la Ghana limezua swali kuhusu ni nchi gani (kama ipo) ya Afrika inaweza kuzalimika kufuata nyayo zake mwaka wa 2023. Kati ya nchi 14 za Kusini mwa Afrika, ni nchi tatu ambazo zina madeni makubwa kwa kutegemea kiwango cha dola kinachozidi 1,000bp [alama za kimsingi]. Hizo zilishuka kutoka nane mwezi Julai," William Jackson, mwanauchumi mkuu wa masoko ibuka katika shirika la Capital Economics la Uingereza aliandika kuhusu kiwango cha madeni Afrika mnamo Desemba 23. "Na nchi hizo tatu ni Zambia na Ghana (tayari zimeshindwa kulipa), na pia Ethiopia (ambayo inaomba kubadilisha madeni chini ya mfumokazi wa kawaida)".

Viwango vya chini vya dhamana nchini Kenya, na ufadhili wa IMF na Benki ya Dunia, vinamaanisha kuwa Kenya inaweza kumudu kulipa madeni siku zijazo, ingawa "inabaki katika hatari kubwa ya kushindwa kulipa madeni".


Rais William Ruto


Rais wa Ghana, Nana Akufo-Addo


Profesa Njuguna Ndung'u

Hatari kubwa ya kushindwa kulipa madeni ya Kenya imezidishwa na kupanda kwa gharama ya ulipaji ambayo kuanzia mwaka wa kifedha unaoisha Juni 2023 imepita gharama ya matumizi kama vile mishahara, kwa madeni kama Eurobond ya kwanza na madeni kutoka China.

Wizara ya Fedha inakadiria gharama ya kulipa madeni itakuwa Sh1.39 trilioni mwaka huu wa kifedha, ambayo ni juu kuliko Sh1.18 trilioni zilizokadiriwa kwa matumizi ya Wizara za Serikali, Idara na Mashirika. Ulipaji huo unakadiriwa kupanda hadi Sh1.67 trilioni katika bajeti ya mwaka wa kwanza ya Rais William Ruto utakaomalizika Juni 2024 hasa kwa kulipa dola za Amerika 2 bilioni (Sh246.60 bilioni) za Eurobond ya kwanza ambayo Kenya ilikopa 2014.

Kenya ilisimamisha shughuli za usimamizi wa madeni za mwaka wa kifedha uliokamilika Juni 2022, hatua ambayo ilinuiwa "kuongeza mfumo wa kukomaa na kupunguza hatari ya kulipa zaidi deni hilo" baada ya kushindwa kupata dola 1.1 bilioni kutoka Eurobond. Hii ilikuwa baada ya wawekezaji kutaka riba ya karibu asilimia 12 mara mbili ya asilimia 6.3 ambayo Kenya ililipa mwaka uliotangulia kwa kiasi sawa.

Kushindwa kupata fedha zilizolengwa kulifanya nchi kusimamisha mpango wa kusimamia deni ambao ulinuiwa kulipa Eurobond ya kwanza ya miaka kumi inayokomaa mwaka wa kifedha unaokamilika Juni 2024.

Viwango vya juu katika masoko ya kifedha duniani "vinatokana na sera ya pesa duniani ya kuongeza viwango kuzuia viwango vya mfumko na pia vita vya Ukraine na Urusi".

Kuongezeka kwa gharama ya kulipa madeni kutoka mwaka ujao wa kifedha kukiwa na viwango vya juu vya riba kulifanya shirika la kukadiria viwango vya madeni duniani la Fitch kushusha thamani ya madeni ya Kenya hadi 'B' kutoka 'B+', katikati ya Desemba kumaanisha kuwa wawekezaji watakuwa wakidai riba ya juu kuliko walivyokuwa wakifanya kwa sababu ya hatari ya juu ya kushindwa kulipa.

Fitch inatarajia Kenya kulipa deni la dola za Amerika 3 bilioni katika mwaka wa kifedha unaokamilika Juni 2023 kupitia ukopaji, zikiwemo dola 900 milioni (Sh110.97 bilioni) kutoka IMF, dola 750 milioni (Sh92.47 bilioni) kutoka Benki ya Dunia kufadhili bajeti na 300 milioni (Sh36.99 bilioni) kutoka Benki ya Maendeleo ya Biashara ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Shirika la Capital Economics la London limetaja Kenya kuwa moja ya nchi zilizo na udhaifu wa kifedha miongoni mwa masoko ibuka Afrika Kusini mwa Sahara kwa kutegemea kipimo cha madeni kwa GDP na uhaba katika kufadhili bajeti. "Serikali itakuwa na kazi kubwa ya kudumisha wawekezaji na mipango yake ya kifedha," akaandika Bw Jackson.

Waziri wa Fedha Njuguna Ndung'u na Gavana wa Benki Kuu ya Kenya Patrick Njoroge waliambia maafisa wa IMF, waliokuwa nchini kati ya Oktoba 25 na Novemba 8, kuwa Kenya "inatafuta shughuli za kusimamia madeni ili kupunguza gharama ya deni na hatari ya ulipaji, hasa kwa kulipa mikopo ya kibiashara inayokomaa".

***-Imetafsiriwa na Benson Matheka***

## UPUNGUFU WA BAJETI

**5%**

Asilimia ya bajeti dhidi ya pato la nchi ambayo ikienda juu huweka nchi katika hatari ya kushindwa kulipa madeni.

**15.9%**

Kiwango cha juu zaidi cha upungufu wa bajeti ya Ghana janga la Covid-19 lilipokuwa kileleni.

**3.9%**

Upungufu wa bajeti ya Ghana dhidi ya pato la nchi mnamo 2017 kabla ya janga la Covid-19.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni




MAGEUZI YA KIKATIBA

# Lazima tuwazime wanasiasa wenye ubinafsi



KWENDO OPANGA

Kwa miaka minne, kuanzia 2018, Bw Raila Odinga alikuwa kigogo katika siasa za Kenya. Alikuwa maarufu hata zaidi ya hasimu wake wa kisiasa aliyegeuka nduguye, Rais Uhuru Kenyatta. Alimpita aliyekuwa Naibu Rais ambaye sasa ni Rais, William Ruto. Aliwazima manaibu rais wa zamani Kalonzo Musyoka na Musalia Mudavadi. Alikuwa kama rais-mwenza.

Hakika, mnamo 2021 nilihoji kuwa Odinga kama mshirika wa rais alikuwa na mamlaka zaidi kushinda alipokuwa Waziri Mkuu.

Mambo yalibadilika ghafla Agosti 15. Kinyume na ilivyotarajiwa, upande uliodunishwa sana wa Ruto uliangusha mrengo uliopigiwa debe zaidi wa Odinga katika uchaguzi wa urais. Muungano wake ulichukua usukani wa Bunge na Musyoka na Odinga wakatupwa katika upinzani, eneo ambapo wamebakia bila furaha tangu 2013.

Na sasa Odinga anatazamiwa kurudi katika eneo ambalo analifahamu vyema, kushinikiza kubadilishwa kwa katiba kupitia baraza la kikatiba. Baraza la kikatiba lilipata umaarufu wake katika enzi za kupigania mageuzi ya kikatiba miaka ya 1990, yakiongozwa na mrengo wa kushoto na wanaharakati.

Baraza la kikatiba ni kundi la wataalamu linaloundwa kwa lengo pekee la kuunda, kutathmini au kurekebisha katiba. Odinga alihoji kwenye mahojiano ya televisheni wiki moja iliyopita kuwa katiba sasa ina miaka 12 na inahitaji kufanyiwa marekebisho kwa sababu Wakenya sasa wanafahamu nguvu na udhaifu wake. Hilary Clinton aliyesema kuwa kila Mkenya ana maoni. Lakini si kila Mkenya ambaye ni mwanasiasa. Huku kila Mkenya akitawaliwa na katiba, kila mwanasiasa anataka kutawala katiba.

Wakati kila Mkenya angependa kuona mageuzi ya katiba yanayozingatia maslahi ya raia, kila mwanasiasa anataka siasa ibadilike kulingana na nafasi yake katika siasa.

Alipokuwa amesukumwa pembeni na Rais Kenyatta na Odinga, Naibu Rais alipinga vikali marekebisho ya katiba yaliyolenga kuunda afisi za kisiasa za kugawanywa miongoni mwa wana na binti za familia maarufu za wanasiasa, maarufu kama 'himaya', katika serikali iliyopanuliwa. Rais Ruto hakika amepanua serikali jinsi tu Kenyatta alivyofanya, bila msingi wa kisheria.

Tayari tumesikia washirika wa Ruto wakipendekeza mageuzi ya katiba ili kuondoa muda uliowekwa wa urais na kuruhusu wanaoshikilia afisi hiyo kubakia mamlakani milele. Wengine wanataka kaunti zaidi zibuniwe bila kujali gharama bali kura.

Wanasiasa walio mamlakani, na walioondoka, wanataka kubadilisha sheria ya kimsingi. Ruto na wasiri wake wanataka Bunge, wanalodhibiti, kuchukua usukani wa mchakato huo. Odinga anataka baraza la kikatiba, ambalo, anasema, ataliunda, kuongoza mchakato huo.

Ni wazi kuwa Rais na serikali anayoongoza watajiepusha kabisa na baraza la kikatiba. Ni wazi kwamba Odinga hadhani Bunge au serikali inahitaji wajibu katika baraza hilo.

Kwa mujibu wa aliyekuwa Jaji Mkuu Willy Mutunga, Katiba ya Kenya 2010 bado haijatekelezwa na kinachotendeka ni kuwa vikosi viwili vinavyowakilishwa na wanasiasa viko katika mvutano mkali kwa sababu upande mmoja unashinikiza na kupigia debe katiba endelevu huku upande mwingine ukiipinga kwa sababu unaichukulia kuwa hatari kwa azma yake ya mamlaka.

Jinsi Mutunga anavyoeleza, hatimaye wahusika watalazimika kuafikiana kutumia katiba inayokubalika na wote, ambayo kwa hakika ndivyo ilivyo Katiba ya Kenya 2010. Lakini ikizingatiwa kuwa hivyo ndivyo inavyokuwa kwa kuwa katiba ni stakabadhi zinazoundwa na wanasiasa, hali hiyo inatia hofu kwa sababu mnamo 2010 Rais alipinga katiba hii huku Odinga akiiunga mkono.

Ni lazima Wakenya wazime juhudi za wanasiasa wanaopigania mabadiliko kwa manufaa yao binafsi.

*kwendo58@gmail.com*

***-Imetafsiriwa na Mary Wangari***

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Mwelekeo ni ule ule, wanasiasa tofauti

# Ni mwanzo mpya, wenye familia mpya za kitajiri



MACHARIA **GAITHO**


Hii ni serikali inazungumza. Kama viongozi wa Kenya Kwanza, tunaungana na wafuasi wetu waaminifu kukaribisha mwaka mpya usio na minyororo ya familia tajiri, washirika wa Serikali na wanaofaidi ukatili wake. Usiku wa manane wa Desemba 31, 2022 utaleta mapambazuko mapya.

Ni wakati wa mwaka ambapo lazima tuwe na nguvu na lengo moja katika kufanya maamuzi ya Mwaka Mpya yanayoashiria mazingira tunayotaka kubuni; mazingira ambayo familia mpya za kitajiri zitabuniwa na Utawala Mpya utaundwa upya Kudhibiti Serikali na kuhakikisha udhibiti wa masuala yote ya kiuchumi kwa manufaa ya watawala wapya waliopo.

Sera za kiuchumi za Bottom-Up zitamweka Hasla na Mama Mboga katika nafasi muhimu sana, kupigania mabaki yatakayoanguka kutoka kwa meza kuu utawala mpya unapoanza mikakati ya kusambaza rasilimali.

Lazima vitisho kutokana na utajiri wa walioendesha serikali iliyopita vipunguzwe kwa kuharibu nguzo zao za kiuchumi, kuuwezesha utawala mpya kupata nafasi. Ni lazima mwaka mpya uandamane na tathmini wazi na za kweli kuhusu jinsi utawala mpya umetenda kazi katika miezi michache ya kwanza, ili kurekebisha makosa yaliyopo na kuturuhusu kuanza upya.

Tunaanza kwa kuangalia historia ndogo. Wakati wa uhuru mnamo 1963, kigezo kikuu kilichotumiwa kwa yeyote aliyetaka nafasi ya uongozi kilikuwa muda ambao mtu huyo alikaa katika magereza ya wakoloni. Kwa bahati mbaya, utawala wa Kenyayatta I ulisaliti kigezo hicho cha maana kwa kujaza nafasi za uongozi na watu walioshirikiana na wakoloni na wasaliti wengine katika harakati za kupigania uhuru.



Mzee Jomo Kenyatta akiapishwa kuwa Waziri Mkuu wa kwanza Kenya mnamo Juni 1, 1963 jijini Nairobi.

Ukombozi wa Pili, mwisho wa utawala wa chama kimoja 1992 na kung'atuliwa kwa Kanu 2002 kulitoa nafasi kwa waliofungwa gerezani, kuhangaishwa na kuhamishiwa ng'ambo kwa kupigania demokrasia na haki za binadamu kutumia vipaji vyao kutumikia nchi. Hata hivyo, wao pia walijipata wakipitwa na watu walioridhiwa kutoka tawala za awali.

Kuibuka kwa utawala wa Jubilee mnamo 2013 kuliingiza serikalini waathiriwa wa taasisi za kibaguzi na ukoloni mamboleo kama vile Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Waliopatikana na makosa ya uhalifu wa kivita walisimama kidete serikalini na hatimaye wakashinda kesi zao. Pia waliondoa vikwazo vya kisheria visivyofaa kwa wanaotaka mamlaka kama vile mahitaji ya uadilifu, ambavyo vingezuia wapiganiaji uhuru kutwaa nafasi za uongozi.

Tena, kwa bahati mbaya, malengo hayo mazuri yalivurugwa utawala wa Kenyatta II ulipobuni ushirikiano na watu waliohalalisha makosa. Utawala wa Kenya Kwanza unalenga kuondoa makosa hayo yote. Walioteuliwa kuwa Mawaziri, Makatibu wa Wizara, katika nafasi za kisiasa, mashirika ya kiserikali, mashirika mbadala, tume za kikatiba, majopo ya rais kati ya mengine watakuwa na nafasi nzuri kama watajihami kukabiliana na uharibifu na uporaji wa mali za umma.

Kuna baadhi walio na kesi za uhalifu au rekodi za awali za uhalifu waliopenya mchakato wa kuwapiga msasa na uteuzi wao kuidhinishwa. Tunapoanza ukurasa wa mwaka mpya, ni lazima watahadharishwe kuwa ni lazima watimize malengo waliyopewa au wajiondoe katika nyadhifa hizo. Hatuwezi kuwa na watu wasio wazalendo katika serikali ya Kenya Kwanza wanaodharau walio na makovu ya juhudi za kupigania ugavi sawa wa rasiilmali na ukombozi wa kiuchumi.

Ni lazima udhibiti wa kiuchumi utolewe katika familia tajiri za Kenyatta na Moi na kuwekwa mikononi mwa mashujaa na wazalendo wa kweli. Watoto wa Mau Mau, Koitalel arap Samoei na Kinjeketile wamesalitiwa, kunyang'anywa mali yao na kufilisishwa tangu uhuru, lakini sasa wamepata nafasi yao.

Siku za kwanza 100 za serikali hii zilitoa nafasi ya kupanga mikakati yake, lakini Mwaka Mpya, utakuwa wa kazi ili kutimiza matumaini na matarajio ya mamilioni ya watu walioonyesha imani yao kwetu. Tutaenda kwa kasi kwa kuwa hatutatatizwa na vikwazo vidogo vidogo vya taratibu za serikali.

Tayari, tunatengeneza bajeti kubwa zaidi katika historia ya Kenya, inayoshinda kwa mbali mafanikio yaliyofikiwa na serikali zilizopita.

Kuhusu pale pesa zitatoka, hilo ni swali la kijinga kwani tunazungumza na serikali marafiki wetu katika nchi za China, Amerika, Ufaransa, Uingereza, Japan na mataifa mengine, kutukopesha pesa nyingi kuliko zilivyokopesha serikali ya Uhuru.

Katika siku chache zijazo, tutachukua udhibiti wa Benki Kuu ya Kenya na kumteua gavana mpya anayeelewa sera za kiuchumi za Hasla kuliko aliyepo.

Sote tunakumbuka miujiza iliyofanywa na gavana wa zamani Eric Kotut katika kutoa kiasi kikubwa cha pesa kwa Rais Daniel arap Moi mapema miaka ya tisini. Pia tunakumbuka kuwa Halmashauri ya Ushuru Kenya (KRA) na mashine za kuchapisha pesa zilizodhibitiwa na CBK zingetoa pesa wakati wowote zilipohitajika.

Hiyo ndiyo sababu tunaweza kusema bila kuogopa kuwa 2023 utakuwa mwaka wa ufanisi na kila mmoja kutajirika. Familia tajiri zitawekwa katika kaburi la sahau na kukabidhi umma utajiri wao huku familia mpya zinazowakilisha Mahasla zikichukua nafasi yake.

*gaithomail@gmail.com*


***- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau***

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Watu wakinunua chakula kabla ya sherehe za Mwaka Mpya jijini Tokyo, Japan mnamo Desemba 29, 2022. PICHA I AFP



Mpiganaji na fahali wa Uhispania Alejandro Talavante akishiriki onyesho la kupigana na fahali katika uwanja wa Canaveralejo wakati wa Tamasha la Cali, jijini Cali, Colombia, mnamo Desemba 28, 2022. PICHA I AFP




Wasafiri watembea barabarani huku wakinyeshewa na theluji mjini Kabul mnamo Desemba 29, 2022. PICHA I AFP



Wapalestina wakipozi kupigwa picha karibu na taa zinazoonyesha 2023 kabla ya sherehe za Mwaka Mpya Jijini Gaza mnamo Desemba 28, 2022. PICHA I AFP



Kijana mfuasi wa dhehebu la Sikh akioga katika bwawa takatifu wakati wa maadhimisho ya kuzaliwa kwa Guru wa 10 wa Sikh, Guru Gobind Singh, katika hekalu ya Amristar mnamo Desemba 29, 2022. PICHA I AFP




Cameron Norrie wa Uingereza akicheza dhidi ya Alex De Minaur wa Australia wakati wa mechi ya tenisi ya United Cup jijini Sydney mnamo Desemba 29, 2022. PICHA I AFP



Mwumini akitazama picha ya aliyekuwa Baba Mtakatifu Benedict XVI katika Kanisa la St Oswald, mjini Marktl, Ujerumani, mnamo Desemba 29, 2022. PICHA I AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

# kurunzi ya afrika

MKONO MREFU WA SHERIA

# JINSI WENYE NGUVU HUISHA



Isabel Jose dos Santos, bintiye aliyekuwa rais wa Angola Jose Eduardo dos Santos

## Mahakama ya Angola yaamuru kutwaliwa kwa mali ya dola 1 bilioni kutoka kwa Isabel dos Santos, aliyetambuliwa kuwa mwanamke tajiri zaidi Afrika

Na ARNALDO VIEIRA

Mahakama ya Upeo ya Angola (ASC), wiki hii iliamuru kutwaliwa kwa mali kadhaa ya binti ya aliyekuwa rais Isabel dos Santos, ya thamani ya dola 1 bilioni, kutokana na ombi la wizara ya Umma.

Kulingana na gazeti la serikali la Jornal de Angola, agizo hilo lilitolewa baada ya kuonekana kwa dalili za uporaji na uhalifu mwingine. "Kuna dalili za uporaji, ushawishi, kushirikisha uchumi katika biashara na ulanguzi wa pesa kunakohitaji adhabu", ikasema, na kuongeza kuwa Isabel anapaswa kufahamishwa tu baada ya mali hiyo kutwaliwa.

Gazeti hilo lilinukuu agizo lililotiwa saini na Jaji Daniel Geraldes, mnamo Desemba 19, ambalo lilisema kuwa "salio lote katika akaunti za benki zilizo na jina la Isabel dos Santos zikiwemo akaunti za kuweka pesa, na zingine za kifedha zinazohusishwa nazo, zikiwemo hisa kwa jina la mshtakiwa Isabel dos Santos, zinafaa kutwaliwa".

Baadhi ya akaunti hizi ziko katika nchi kama Msumbiji, Cape Verde na Sao Tome and Principe, ikaongeza.

Mahakama pia imeamuru kuzuiliwa kwa asilimia 70 ya hisa katika kampuni ya mawasiliano ya Msumbiji, Mstar, ambazo "zinafaidi" Isabel dos Santos na ikaagiza kutwaliwa kwa asilimia 70 ya hisa za mshtakiwa katika kampuni ya Upstar Comunicação.

Mahakama pia iliagiza kutwaliwa kwa asilimia 100 ya hisa za kampuni za Unitel katika nchi ya Cape Verde na Unitel STP katika Sao Tome and Principe, ambazo mfanyabiashara huyo mwanamke wa Angola anamiliki. Embalvidro, Unitel International Honding na Unitel International ni kampuni zingine zilizotajwa katika agizo hilo la mahakama.

Isabel dos Santos, 49, ambaye wakati mmoja aliheshimiwa kwa kuwa mwanamke tajiri Angola na Afrika, sasa anatazama serikali ya Angola ikimgeuka. Isabel, ambaye pia ana uraia

Endelea Uk 12

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Kutoka Uk 11

wa Urusi, amekuwa akiheshimiwa kwa muda mrefu katika nchi yake, hasa wakati wa utawala wa miaka 38 wa baba yake.

Alizaliwa Baku, Azerbaijan, wakati wa enzi za vita baridi na mama yake, Tatiana Kukanova, ni raia wa Urusi aliyekutana na baba yake José Eduardo dos Santos wakisoma chuo kikuu.

Rais dos Santos alitawala Angola kutoka 1979 hadi 2017. Akiwa mamlakani, dos Santos alitawala nchi hiyo kama kampuni yake ya kibinafsi. Washirika wake wa karibu, wakiwemo watu wa familia yake, walilaumiwa kwa kupora mali za taasisi za serikali.

Ndoa ya Rais Eduardo dos Santos na Kukanova haikudumu. Mnamo 1979, Kukanova alihamia London akiwa na binti yake Isabel ambako alisomea shule za kifahari akiwa tineja ya King's College London, alikopata digrii ya uhandisi na kukutana na aliyekuwa mumewe baadaye, Sindika Dokolo.

Bw Dokolo alikuwa mfanyabiashara tajiri wa Congo. Kutokana na kuishi Uingereza kwa miaka mingi - 18, Isabel, ambaye pia anazungumza kwa ufasaha Kiingereza, Kifaransa, Kitaliano, Kireno, Kirusi na Kihispania, pia ana uraia wa Uingereza.





Mwenye simu akionyesha nembo ya polisi wa Interpol katika picha hii iliyopigwa jijini Kharkiv, Ukraine, mnamo Juni 16, 2022. Isabel dos Santos amekuwa akiandamwa na Interpol kwa muda. PICHA I MAKTABA

# Isabel dos Santos: Kutoka shujaa hadi mshukiwa

Mnamo 1997, alifungua mkahawa maarufu unaojulikana kama Miami Beach aliporudi Angola na kuanza kupata pesa. Mnamo 2001, aliwekeza katika kampuni za Angola na Ureno na akafungua kampuni zake binafsi za mawasiliano (Unitel na Zap).

Mnamo Desemba 2002, akiwa na umri wa miaka 29, Isabel alifunga ndoa na Bw Dokolo, aliyekuwa na umri wa miaka 30 na wawili hao wakawa washirika wa biashara.



Aliyekuwa Rais wa Angola Jose Eduardo dos Santos akipungia mkono umati wa watu wakati wa kampeni eneo la Kilamba Kaixi, nje ya mji wa Luanda, mnamo 2012. Tangu alipoondoka mamlakani nchini humo, sifa za kisiasa na kiuchumi za binti yake Isabel zimeshuka kwa haraka. PICHA I AFP

Alipofika umri wa miaka ya 30, Isabel alikuwa akimiliki nyumba za kifahari katika miji mikuu ya Ulaya kama London na Lisbon.

Hasa, Forbes ilimtangaza Isabel mwanamke tajiri zaidi Afrika na bilionea wa kwanza mwanamke barani, aliyekuwa na utajiri wa thamani ya dola 3.5 bilioni mnamo 2013. Baadaye 2016, Isabel aliteuliwa na baba yake kuwa mkuu wa Sonangol, kampuni ya mafuta inayomilikiwa na serikali ya Angola. Mwaka uliofuata, mrithi wa baba yake alimtimua kutoka wadhifa huo.

Lakini mwaka jana, Jarida la Forbes lilisimulia jinsi aliyekuwa wakati mmoja mwanamke tajiri zaidi barani alivyofilisika. Katika makadirio yake, Forbes ilisema Isabel si bilionea tena, na likamuondoa katika orodha yake mpya iliyotolewa 2021 ya watu matajiri Afrika.

Hakuhesabiwa kuwa bilionea kwa kuwa baba yake hakuwa mamlakani, himaya yake ilikumbwa na mashtaka ya ufisadi, mali yake ilizuiliwa na mahakama katika nchi tatu tofauti na kesi zilimgharimu mamia ya dola kwa kutolipa madeni katika nchi ya nne.

Wakati huo huo, inaonekana malkia huyo wa Angola analipia makosa ya baba yake ambaye alimtaja kuwa chanzo cha bidii yake. Mnamo 2020, muungano wa Wanahabari Wapekuzi Ulimwenguni wenye makao yake jijini New York, baada ya kushirikiana na magazeti ya kimataif, ulichapisha faili kadhaa za madai yaliyoonyesha jinsi Dos Santos alipora mamilioni ya dola ya pesa za umma na kuzificha katika akaunti ng'ambo katika makala yaliyoitwa "Luanda Leaks".

Mwaka wa 2020 utakuwa mwaka wa kumbukumbu nyingi za huzuni kwa Isabel. Bw Dokolo alikufa akiwa Dubai Oktoba 29 akiwa na umri wa miaka 48. Kulingana na watu wa familia yake, alikufa kwenye ajali ya barabarani pwani ya Dubai. Mnamo Januari, maafisa wa Angola walishtaki wawili hao kwa makosa ya ulanguzi wa pesa na uporaji. Isabel alikanusha madai hayo mara nyingi.

Mnamo Agosti, hakuweza kuhudhuria mazishi ya baba yake jijini Luanda kwa sababu aliogopa kukamatwa na maafisa wa serikali ya Angola kujibu mashtaka dhidi yake.

Mwezi uliopita, Mwanasheria Mkuu wa Angola, alithibitisha kwamba Shirika la Kimataifa la Polisi wa Kupambana na Uhalifu (Interpol) lilikuwa limetoa kibali cha kimataifa cha kumkamata Isabel dos Santos.

Kwa upande wake, Isabel dos Santos alitaja tangazo hilo kuwa mateso ya kisiasa. "Nafikiri leo inaeleweka vyema kuhusu kinachoendelea kweli na hakuna shaka kwamba tunakabiliwa na mateso ya kisiasa," akasema akihojiwa na shirika la habari la CNN nchini Portugal, mnamo Novemba.

"Kwa kutazama Angola na mfumo wetu wa sheria, ni rahisi kuelewa kwamba Mwanasheria Mkuu anapokea maagizo moja kwa moja kutoka kwa Rais. Hii ni tofauti na baadhi ya nchi, ambako mwendesha mashtaka ni huru, au anategemea taasisi nyingine," akaongeza.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

KUONDOLEWA KWA MASHARTI YA COVID-19

# CHINA YAZUA HOFU DUNIANI



Mzee akipokea chanjo ya Covid-19 mjini Qingzhou katika Jimbo la Shandong, mashariki mwa China mnamo Desemba 16, 2022.
PICHA I AFP

## Wasiwasi baada ya Beijing kuondoa masharti ya janga licha ya ongezeko kubwa zaidi la maambukizi ya Covid-19 ulimwenguni

• Beijing, AFP

HATUA ya ghafla ya China ya kuondoa masharti ya kudhibiti Covid-19 imezua wasiwasi kote ulimwenguni, huku Amerika ikisema huenda ikikataa wasafiri kutoka China baada ya nchi hiyo kuondoa agizo kuwa watu wanaowasili kutoka nje wawekwe kwenye karantini.

Jumatatu jioni, China iliondoa amri ya karantini kwa wasafiri wanaowasili nchini humo kuanzia Januari 8. Hilo ndilo sharti la mwisho lililokuwa limebakia miongoni mwa masharti makali ya kudhibiti Covid na kuondolewa kwake kunaashiria kukomeshwa kwa baadhi ya masharti makali zaidi ya mipakani duniani.

Raia wa China walishangilia kuondolewa kwa sharti hilo, wengi wakiharikisha kununua tiketi za kusafiri nje. Hatua hiyo ilichangia kupanda kwa bei ya tiketi hizo.

Hospitali na maeneo ya kuchomea maiti kote nchini China zinaendelea kulemewa na idadi kubwa wa waathiriwa Covid-19, hasa ya wakongwe.

Wanahabari wa AFP waliona wagonjwa wengi wakongwe wa Covid-19 wakilala kwenye machela katika wadi za hospitali mjini Tiajini, kilomita 140 kusini magharibi mwa Beijing, Jumatano.

Wahudumu wa afya "karibu wote" wanatarajiwa kuendelea kufanyakazi licha ya kupatikana na virusi vya ugonjwa huo, daktari moja alisema.

Nchi zingine zimeelezea hofu

Endelea Uk 14

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

# Jicho la tahadhari kwa Beijing

Kutoka Uk 13

kuhusu uwezekano wa aina mpya ya virusi vya Covid-19 kutokea huku China ikipambana na ongezeko kubwa la maambukizi kuwahi kushuhudiwa ulimwenguni.

Maafisa wa Amerika walisema Jumanne jioni wanafikira kuweka masharti ya kuzuia wasafiri kutoka China kuingia humo.

Hiyo ni baada ya nchi kadhaa, ikiwemo Japan na India kuanzisha sharti la wasafiri wote kutoka China kupimwa kubaini kama wana virusi vya corona au la. "Kuna hofu kubwa miongoni mwa jamii za kimataifa kuhusu ongezeko la maambukizi ya Covid-19 yanayoshuhudiwa nchini China na kutokuwepo kwa data muhimu kuhusu ugonjwa huo kutoka kwa serikali ya nchi hiyo," wakasema maafisa wa Amerika.

Amerika inafikira kuchukua "hatua sawa" na zile ambazo zimechukuliwa na Japan na Malaysia, wakaongeza.

Taiwan, kisiwa kinachojitawala na ambacho China inadai kumiliki, ilisema Jumatano itakagua wasafiri wote kutoka bara kubaini iwapo wana virusi au la.

Hatua ya China kulegeza masharti imekomesha hatua zingine za kudhibiti Covid za kupima watu, kuzuia watu kuingia na kutoka maeneo fulani na kuwekwa watu karantini kwa muda mrefu. Masharti hayo yamekwamisha uchumi wa China na kuchochea maandamano makubwa nchini humo. " Kwa sasa, utayarishaji wa ripoti kuhusu hali ya janga hilo China unaendelea vizuri," msemaji wa wizara ya mashauri ya kigeni Wang Wenbin akasema Jumatano.

"Habari za kuongeza chumvi, kuharibu sifa na uingiliaji wa kisiasa wenye malengo mabaya hautaficha ukweli," Wang akaongeza, akitaja vyombo vya habari vya Magharibi vinavyoripoti kuhusu ongezeko la Covid nchini China kuwa "vinavyopendelea."

Tangu Machi 2020 wasafiri wote wanaowasili China walilazimika kuwekwa karantini. Muda wa kutengwa ulipunguzwa kutoka wiki tatu hadi wiki moja mnamo Juni, na siku tatu mwezi uliopita.

Kusitishwa kwa sharti hilo kuanzia Januari pia kutapelekea Covid-19 kushushwa daraja hadi magonjwa ya kuambukiza ya "Kiwango B" na kuruhusu serikali kutekeleza masharti mepesi. Maafisa wa Idara ya Uhamiaji China Jumanne walisema wataanza tena kutoa paspoti za watalii kuanzia Januari 8, baada ya miaka ya masharti makali.

Ongezeko la maambukizi msimu wa baridi linajiri kabla ya sikukuu za kitaifa mwezi ujao ambapo mamilioni ya watu wanatarajiwa kusafiri makwao kujumuika na jamaa zao.

Serikali ya China imesema kiwango cha maambukizi hayo sasa ni "vigumu" kubainika huku wakipunguza vigezo vya kutambua vifo kutokana na Covid.

Kituo cha Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa China kiliripoti visa vipya 5,231 vya Covid-19 na vifo vitatu nchini humo Jumatano. Hii inaonekana kuwa idadi ya chini ikizingatiwa kuwa watu hawahitajiki kujulisha serikali kuwa wameambukizwa.

Serikali inatumia data kutoka kwa chunguzi za mitandaoni, idadi ya wanaofika hospitalini, hitaji la dawa za kupunguza homa na simu za dharura kufidia ukosefu wa takwimu rasmi," afisa wa kituo hicho, Yin Wenwu, akaambia wanahabari Jumanne.

Huku nchi hiyo ikukumbwa na uhaba wa dawa, maafisa wa jiji la Beijing wanapanga kusambaza dawa ya Covid aina ya Paxlovid katika hospitali na kliniki za kijamii. Bado ni vigumu sana kwa dawa hizo kupatikana kwa watu wa kawaida.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Picha hii ya maktaba iliyopigwa Septemba 18, 2022 inaonyesha wafanyakazi katika uwanja wa ndege wa Yantai, China wamevaa mavazi ya kujikinga, wakishughulikia ndege iliyotua kutoka ugenini. China imeondoa sharti la kuweka karantini wanaofika humo na kupiga hatua nyuma miaka kadhaa ya masharti makali ya kudhibiti virusi vya Corona. PICHA I AFP

# Hatua ya China yazua hofu ya mfumko wa bei

• Hong Kong, AFP

Mauzo ya hisa katika masoko ya Asia yalipungua Jumatano kufuatia kushuka kwa mauzo katika Soko la Hisa la Amerika baada ya China kuondoa masharti ya kudhibiti Covid na kuzua hofu ya mfumko wa bei za bidhaa.

China imeondoa ghafla masharti hayo ambayo yametenga nchi hiyo na maeneo mengine duniani kwa miaka mitatu iliyopita.

Mnamo Jumatatu, China ilitangaza kuwa itaacha kuweka karantini wageni wanaofika nchini humo kuanzia Januari 8, hatua ya majuzi zaidi ya kulegeza masharti yake ya Covid baada ya kuondoa vipimo vya lazima na kuacha kufunga maeneo mbalimbali mapema mwezi huu.

Hatua hiyo imeleta matumaini ya kufufuka kwa uchumi wake lakini pia kuzua hofu ya mfumuko wa bei za bidhaa.

Hatua ya China kufungua uchumi kukiwa ongezeko la maambukizi ya Covid imezua wasiwasi, huku Amerika na mataifa kadhaa yakisema huenda yakazuia watu kutoka China na kuanza vipimo vya lazima kwa wanaofika.

"Ingawa kufunguliwa kwa uchumi wa China kutaimarisha uchumi wa dunia, kunaweza kusababisha madhara, akasema Stephen Innes wa shirika la SPI Asset Management.

"Habari njema ni kuwa mfumuko wa bei utapungua China itakapoanza kusambaza bidhaa za bei rahisi kote duniani," akasema Innes.

"Lakini pia tatizo ni kuwa uchumi ukiimarika robo ya kwanza ya mwaka ujao hali ya China ya kutaka malighafi na kawi itasababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa hizo na kuathiri viwango vya riba katika Benki Kuu ya Amerika (FED) na Benki Kuu ya Ulaya (ECB). Hasa, kufungua upya uchumi huo ni kurudisha mfumuko kwa kiwango fulani."

Wiki iliyopita, maelezo mapya yalionyesha kushuka kwa mfumko wa bei Amerika, lakini maelezo hayo hayakuwa ya kuridhisha. Macho yote yataelekezwa hatua ambayo FED itachukua kuondoa hofu hiyo na uwezekano wa kudidimia kwa uchumi kutokana na ongezeko la gharama ya mikopo.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Makombora aina ya Patriot 'si suluhisho'



• Washington

Hatua ya Amerika ya kuipatia Ukraine makombora aina ya Patriot ni ishara kubwa ya kuunga mkono nchi hiyo na itaboresha juhudi zake za kujilinda dhidi ya Urusi, lakini wataalamu wanasema hayatakuwa na athari kubwa kivita.

Makombora ya Patriot "si suluhisho" dhidi ya makombora ambayo vikosi vya Urusi vimekuwa vikitumia kuishambulia Ukraine, kulingana na Ian Williams wa Mradi wa Makombora ya Kujilinda katika Kituo cha Mafunzo ya Kimkakati na Kimataifa, jijini Washington.

Lakini yataongeza kiwango cha ulinzi cha Ukraine kwa sasa na pia kuisaidia kujilinda dhidi ya makombora ya masafa mafupi ambayo maafisa wa nchi za Magharibi wanafikiri Urusi inayapata kutoka Iran, akasema Williams. "Ni muhimu kuwa na aina tofauti ya ulinzi unapokabiliana na mashambulio makali ya angani," akaambia AFP.

Hatua hiyo pia itatoa ujumbe mkali kwa washirika wa Urusi na Ulaya kuwa Amerika iko tayari kuisaidia Ukraine kwa silaha za kisasa za kivita kukabili Urusi.

Kombora la Patriot MIM-104 hurushwa angani kutoka ardhini na awali liliundwa kudungua ndege zinazopaa juu sana kutoka ardhini. Liliundwa upya miaka ya themanini kutokana na tishio la kombora linaloweza kusafiri masafa marefu. Makombora ya Patriot yalionyesha uwezo wake dhidi ya Scud kutoka Urusi yaliyotumiwa na Iraq wakati wa Vita vya Kwanza vya Ghuba.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# AINA MPYA YA KUKU KUZAA WA KIKE TU, HAKUNA JOGOO



**Kuku aina ya Brahma alikuwa wa pili bora katika kiwango chake kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Mombasa mwaka huu katika picha hii iliyopigwa Novemba 4, 2022.** PICHA I KEVIN ODIT

• Jerusalem

Wanasayansi wa Israel wamezalisha aina ya kuku ambao mayai yao yanaangua kuku wa kike pekee, ufanisi ambao unaweza kusaidia kumaliza uuaji wa vifaranga wapatao bilioni saba wa kiume kila mwaka duniani.

Vifaranga hao, wanaotokana na mayai, huharibiwa kwa wingi kwa kunyimwa hewa au kuuawa kwa sababu hawafai kwa nyama na pia hawatagi mayai.

Wanaharakati wa haki za wanyama wamelalamikia hatua hiyo wakisema ni ya kikatili, na imepigwa marufuku katika nchi kadhaa za Ulaya.

Marufuku nchini Ujerumani yalianza mwaka huu. Wakulima wa Ufaransa wanatarajiwa kuanza kufuata sheria hiyo mpya mwaka huu.

Kundi la watafiti kutoka kituo cha Volcani cha Shirika la Utafiti wa Kilimo Israel wametumia uchujaji wa jeni kuunda aina mpya ya kuku wanaozaa vifaranga wa kike pekee. Wanasema hii ndiyo njia pekee ya kuzuia uuaji wa vifaranga wa kiume kwa wingi kote duniani.

"Hii ni suluhu ya kwanza duniani ambayo ni rahisi kwa wadau wa sekta hii kutekeleza," kiongozi wa utafiti huo, Yuval Cinnamon, ambaye ni mtaalamu katika kituo cha Volcani akaambia AFP.

Kituo cha Volcani kiliunda aina hiyo kufuatia utafiti wa miaka saba kikishirikiana na kampuni ya Huminn inayomilikiwa na Amerika na Israel.

Teknolojia hiyo inahusu kubadilisha kuku wanaotaga mayai hivi kwamba mayai yake yanayobeba kiinitete cha kiume hayafikii kiwango cha kuangua. "Baada ya kutungisha, kiinitete cha kiume hakikui ilhali kiinitete cha kike kinakua kama kawaida bila kubadilishwa jeni na kuagua kama kawaida," akaeleza Cinnamon.

"Ufanisi huu utatoa suluhisho la hakika kwa kile ambacho pengine ni tatizo kuu kuhusu maslahi ya wanyama katika ulimwengu siku hizi," akaongeza.

Mbali na kufaidi haki za wanyama, teknolojia hiyo inaweza kufaidi wanaozalisha kuku kwa kuokoa nafasi na kawi inayohitajika kuendesha viangulio huku ikipunguza gharama kwa kiwango kikubwa.


"Inagharimu dola moja kuua vifaranga wa kiume wasiohitajika, kwa hivyo hiyo ni kuokoa bilioni saba kwa mwaka," akasema Cinnamon.

Kampuni ya Huminn imebashiri kuwa manufaa ya kibiashara kutokana na teknolojia hiyo yanaweza kupatikana baada ya miaka miwili.

Katika mkutano wa Oktoba, mawaziri wa kilimo wa Muungano wa Ulaya walisema watapiga marufuk uuaji wa vifaranga wa kiume wakingojea matokeo ya uchunguzi wa athari zake.- AFP

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM